

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA VWAWA-MLOWO (VWAWA-MLOWO WSSA) KWA MWAKA 2018/19 – 2020/21

Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-006-2018/2019

Mnamo tarehe 16 Februari 2019 Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi yaliyokamilika kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Vwawa-Mlowo (Vwawa-Mlowo WSSA) ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake za maji safi kwa mwaka 2018/19 hadi 2020/21. Majedwali namba 1 hadi 3 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na bei zinazopendekezwa

Jedwali Na 1: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi kwa Uniti moja ya ujazo)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zinazopendekezwa					
	2017/18	Mabadiliko (%)	2018/19	Mabadiliko (%)	2019/20	Mabadiliko (%)	2020/21
Majumbani	395	287%	1,530	0.3%	1,535	6%	1,620
Taasisi	400	285%	1,540	0.0%	1,540	7%	1,650
Biashara	390	340%	1,715	0.3%	1,720	2%	1,760
Viwanda	500	284%	1,920	0.0%	1,920	2%	1,950
Magati	1,000	150%	2,500	0.0%	2,500	0%	2,500

Jedwali Na.2: Ada ya Maunganisho ya Huduma ya Maji ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi kwa Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa		Ada Zinazopendekezwa				
	2017/18	Mabadiliko (%)	2018/19	Mabadiliko (%)	2019/20	Mabadiliko (%)	2020/21
Majumbani	46,500	8%	50,000	4%	52,000	4%	54,000

Taasisi	47,000	6%	50,000	4%	52,000	4%	54,000
Biashara	47,500	5%	50,000	4%	52,000	4%	54,000
Viwanda	48,500	3%	50,000	4%	52,000	4%	54,000

Jedwali Na.3: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa huduma)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Zinazopendekezwa					
	2017/18	Mabadili ko (%)	2018/19	Mabadili ko (%)	2019/20	Mabadili ko (%)	2020/21
Majumbani	5,500	82%	10,000	0%	10,000	0%	10,000
Taasisi	5,500	82%	10,000	0%	10,000	0%	10,000
Biashara	5,500	82%	10,000	0%	10,000	0%	10,000
Viwanda	5,500	82%	10,000	0%	10,000	0%	10,000
Magati	5,500	82%	10,000	0%	10,000	0%	10,000

Kwa Mujibu wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vwawa-Mlowo, sababu za kuomba marekebisho ya bei za huduma zake ni pamoja na uhitaji wa mapato ya kutosha kumudu ongezeko kubwa la gharama za uendeshaji na matengenezo, kugharamia miradi ya uwekezaji na ununuzi wa vifaa pamoja na kulipa tozo mbalimbali zilizopo kisheria.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Jumane, tarehe 16 Aprili 2019** katika **Ukumbi wa Shule ya Sekondari Vwawa** uliopo Vwawa, Mbozi kuanzia saa **4:00 asubuhi**. Lengo la mkutano huo ni kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia huduma zinazodhibitiwa na EWURA, wateja wa Mamlaka ya Maji Vwawa-Mlowo, na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonesha hapo juu **ifikapo tarehe 19 Aprili 2019**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi za **EWURA KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI, GHOROFA YA SITA, JENGO LA NHIF; MTA A WA KARUME, MBEYA** au **OFISI ZA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA VWAWA-MLOWO** zilizopo **VWAWA, MBOZI**.

Imetolewa na:
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
(EWURA)

29 Machi 2019